Shule za msingi za Serikali Dar es Salaam: Vyoo vibovu, michezo kidogo

Matokeo muhimu

- Shule nyingi zinakabiliwa na mazingira yasiyofaa kiafya
- Shule nyingi hazina viwanja vya michezo vinavyofaa na vinavyotosheleza mahitaji

Utangulizi

Tangu mwaka 2002, Serikali ya Tanzania imekuwa ikitekeleza Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) wenye madhumuni mawili makuu: kupanua zaidi upatikanaji wa elimu na kuinua viwango vya ubora wake. Wakati ambapo mafanikio makubwa yamepatikana katika kupanua upatikanaji wa elimu ya ngazi ya msingi, suala la kuinua viwango vya ubora bado linaendelea kuwa changamoto kubwa.

Dar es Salaam ni jiji kubwa kuliko miji yote nchini, na ni jiji lililo karibu zaidi na mahali sera zinapotungwa, hivyo mara nyingi inafikiriwa kuwa hali katika jiji hili ni bora zaidi kuliko mahali pengine. Hata hivyo, vyombo vya habari vimekuwa vikichapisha taarifa zinazotoa ushahidi unaoonesha kuwa shule za Dar es Salaam hazina vifaa vya kujifunzia na kufundishia na kwamba kuna haja kubwa ya kurekebisha hali hiyo. Kutokana na hali hii, Uwazi ilifanya utafiti kati ya mwezi Agosti na Desemba 2010 uliotathmini ubora wa huduma na vifaa/nyenzo katika sampuli ya shule za msingi 40 katika manispaa tatu za Dar es Salaam: Ilala, Kinondoni, na Temeke.

Muhtasari huu ni wa pili katika mfululizo wa machapisho kuhusu ubora wa shule za msingi za Serikali katika mkoa wa Dar es Salaam. Matokeo yanaonesha kwamba shule nyingi za Serikali za Dar es Salaam hazina viwanja bora vya michezo na zinakabiliwa na mazingira duni kwa afya.

Jambo la 1: Huduma za kiafya katika shule nyingi hazitoshelezi

Lengo la Serikali kuhusu huduma za kiafya mashuleni ni kuwa na choo cha shimo kimoja kwa wanafunzi 20 wasichana na choo cha shimo kimoja kwa wanafunzi wavulana 25. Katika shule zilizotafitiwa hali inaonyesha kwamba lengo hili liko mbali sana kufikiwa (tazama Kielelezo cha 1). Wastani wa uwiano wa mwanafunzi kwa choo cha shimo kimoja ni wanafunzi 90 (90:1). Shule 11 tu kati ya shule 40 (asilimia 27.5) zina uwiano wa wanafunzi pungufu ya 47 kwa shimo moja la choo. Kati ya shule hizi, ni shule 6 tu (shule za msingi Gerezani, Buguruni Viziwi, Oysterbay, Muhimbili, Mnazi Mmoja na Amana) ndizo zina vyoo vya kutosha kwa kuzingatia lengo la taifa.

Muhtasari huu umeandaliwa chini ya uangalizi wa Rose Aiko wa Uwazi iliyopo Twaweza-HivosTanzania.

Uwazi, S.L.P. 38342, Dar es Salaam, Tanzania.
Simu +255 22 266 4301. Nukushi +255 22 266 4308.
Baruapepe: info@uwazi.org. Tovuti: www.uwazi.org
Umetolewa Mei, 2011.

Idadi ya matundu ya vyoo na uwiano wake kwa wanaafunzi ni sehemu tu ya kipimo cha hali ya huduma za kiafya ilivyo katika mashule. Hali inaonesha kuwa vyoo vingi pia haviko katika hali nzuri. Mifano ya kusikitisha imeonekana hasa katika Shule ya Msingi Msisiri iliyopo wilayani Kinondoni na Shule ya Msingi ya Vijibweni katika wilaya ya Temeke. Vyoo 10 vya plastiki vilivyotolewa msaada na wasamaria wema katika Shule ya Msingi ya Msisiri kamwe havitoshi kwa wanafunzi 1,173 waliopo shuleni hapo. Lakini pia angalau hapo Msisiri kuna huduma ya maji ya DAWASCO, shule ya Msingi Vijibweni haina bahati kama hiyo. Shule ina wanafunzi 2,126, mashimo ya vyoo 12, na katika shule hiyo hakuna maji ya bomba wala ya kisima. Kwa mujibu wa mwalimu mkuu, hapo shuleni wanafanya kile kinachowezekana, na wanategemea uhusiano wao mwema na majirani ambao wakati mwingine huipatia shule maji.

Wakati mwingine, vyoo ni vichafu mno kiasi kwamba wavulana wa madarasa ya chini ya shule za msingi wamebuni njia ya kujisaidia wakiwa wamesimama nje ya vyoo hivyo (tazama picha).

Kielelezo cha 1: Idadi ya wanafunzi wanaoshirikiana shimo moja la choo na mgawanyo wa shule zinazohusika



Chanzo cha takwimu: Uwazi, 2010

Jambo la 2: Shule moja katika kila shule nne haina kiwanja cha michezo

Katika mtaala wa Elimu ya Msingi, kuna somo linalohusiana na michezo linaloitwa '*Haiba na Michezo'.* Ingawa shule nyingi zinadai kufundisha somo hilo, shule nyingi hazina viwanja vya michezo vinavyofaa na vifaa vya michezo. Shule zikiwa zinakabiliwa na matatizo mengine mengi, michezo inapewa nafasi ndogo na mara nyingi haipewi hadhi inayostahili. Shule moja katika kila shule nne zilizotafitiwa imeripoti kuwa haina kiwanja cha michezo. Pamoja na hili, shule nyingi kati ya zile zenye viwanja vya michezo zimeonesha kuwa viwanja hivyo haviko katika hali inayokidhi mahitaji ya michezo kutokana na kukosa vifaa muhimu.

Kielelezo cha 2: Je, shule ina kiwanja cha michezo?



Chanzo cha Takwimu: Uwazi, 2010

Viwanja vingi ni vya wazi na zaidi viko kwa ajili ya mpira wa miguu na/au riadha. Katika Shule ya Msingi Boma iliyo katika manispaa ya Ilala, inasemekana kuwa kiwanja kimevamiwa na majirani na hivyo hakiwezi kutumika tena kwa michezo ya shule.

Hitimisho

Huduma bora ya choo ni muhimu kwa mazingira mazuri ya kujifunza na inapaswa kupewa kipaumbele katika shule zote. Suluhisho moja linaloweza kuangaliwa ni kuhakikisha kuwa huduma za kiafya (vyoo na maji ya bomba/visima) vinakuwepo kabla shule hazijaanzishwa, na kwamba vitu hivyo vinafanyiwa matengenezo kila mwaka.

Hivi karibuni, Serikali ilirudisha upya masomo ya michezo katika mitaala ya shule na mashindano ya michezo ili kuwatia moyo vijana wenye vipaji mbalimbali kujiendeleza kimichezo, na kufanya mazingira ya kujifunza kuwa ya kuvutia zaidi. Ili kufanikisha azma hii, Serikali inahitaji kuhakikisha kuwa shule zote zina viwanja vya michezo vilivyo katika viwango vizuri na vinavyotosheleza mahitaji; kwamba shule zinapata au kuwa na angalau kiasi cha msingi cha vifaa vya michezo kila mwaka; na kwamba eneo la shule linalindwa, kwa mfano, kwa kujengewa uzio ili kuzuia majirani kuvamia nafasi zilizotengwa kwa ajili ya michezo. Vinginevyo ahadi ya Serikali ya kufufua michezo mashuleni haitafanikiwa kikamilifu.

Kiambatisho: Shule za msingi za Serikali zilizotembelewa katika utafiti

Wilaya ya Temeke (16)	Wilaya ya Ilala (13)	Wilaya ya Kinondoni (11)
Vijibweni	Buguruni Moto Mpya	Kawe A
Mji Mwema	Boma	Kumbukumbu
Mivinjeni	Amana	Mapambano
Toa Ngoma	Buguruni Viziwi	Mbuyuni
Kibada	Msimbazi Mseto	Oysterbay
Chang'ombe	Gerezani	Kinondoni
Geza Ulole	Muhimbili	Msisiri
Mtoni Kijichi	Ukonga	Mlimani
Kimbiji	Buguruni Moto	Bunju A
Kurasini	Buguruni	Mtongani
Kibugumo	Mnazi Mmoja	Kunduchi
Tandika	Uhuru Wasichana	
Mgulani	Bunge	
Mikwambe		
Kigamboni		
Mbagala		

Chanzo cha Takwimu

Muhtasari huu ni sehemu ya ufuatiliaji wa wananchi unaofanywa kupitia Uwazi, www.uwazi.org. Takwimu zilikusanywa kupitia utafiti wa ufuatiliaji ulioendeshwa kati ya mwezi Agosti na Desemba 2010. Takwimu zote zinaweza kupatikana kutoka Uwazi.